SWALI: Je! Mke wa ujana ni yupi.. Je! siruhusiwi kumwacha Rafiki yangu wa kike (Girlfriend) au wa kiume (Boyfriend) na kwenda kuwa na mahusiano na mwenzi mwingine, kwasababu yule wa kwanza ndio mwenzi wa ujana wangu?

JIBU: Mke wa ujana kama inavyozungumziwa katika biblia sio Rafiki wa kike (GF) Bali ni mke ambaye ulishafunga naye ndoa tangu ukiwa kijana, hadi sasa umeshakuwa mtu mzima au umeshazeeka. Huyo mke uliyenaye sasa ndio anaitwa mke wa ujana wako.Ulikuwa naye tangu enzi na enzi.

Neno hilo utakutana nalo katika vifungu hivi,

> *Malaki 2:14 “Lakini ninyi mwasema, Ni kwa sababu gani? Ni kwa sababu Bwana amekuwa shahidi kati ya wewe na mke wa ujana wako, uliyemtenda mambo ya hiana, angawa yeye ni mwenzako, na mke wa agano lako”.*

> *Mithali 5:18 “Chemchemi yako ibarikiwe; Nawe umfurahie*

> *mke wa ujana wako”.*

Hivyo kulingana na swali lako ni kwamba, hupaswi kumwacha mke wako ambaye ulikuwa naye tangu ujanani, ukaenda kuoa mwingine, hiyo ni dhambi kubwa sana, vilevile hupaswi kumwacha mume wako, uliyeolewa naye tangu ujanani mwako, ukaenda kuolewa na mume mwingine hiyo ni dhambi. Utakuwa unafanya dhambi ya uzinzi, haijalishi hakuvutii tena kwako kiasi gani.

Lakini hapo haizungumzii, Boyfriend au Girlfriend. Katika Imani ni kosa mtu kuishi na msichana au mvulana, au kuwa na mahusiano yoyote ya kimapenzi na mtu ambaye bado hajawa mke/ mume wake.

Bwana akubariki.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema,

Kwa maombezi/Ratiba za ibada/ Ushauri/ Maswali.
Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

pia kama utapenda uyapate mafundisho haya kwa njia ya Whatsapp au email basi tutumie ujumbe kwenye namba hizo hizo.

Mada Nyinginezo:

> *MZAZI, JALI MAISHA YA KIROHO YA MTOTO WAKO.*

> *Je! Daudi hakuwa mtoto wa ndoa wa Yese? (Zab 51:5)*

> *UFUNUO: Mlango wa 14*

> *ITAKUFAIDIA NINI?*

> *Fumo ni nini kama tunavyosoma katika biblia? (Hesabu 25:7)*

Rudi nyumbani

Share on:
WhatsApp